# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

### SEHEMU YA PILI
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI WA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU NA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU, NAM. 10 YA 2009

3. Kusomwa.
4. Marekebisho ya kifungu cha 2.
5. Marekebisho ya kifungu cha 10C.

### SEHEMU YA TATU
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR, NAM. 3 YA 2015

6. Kusomwa.
7. Marekebisho ya kifungu cha 2.
8. Kuongeza kifungu kipya cha 66A.
9. Kuongeza kifungu kipya cha 69A.
10. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 86.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) MAFUTA NA GESI ASILIA, NAM. 6 YA 2016**

11. Kusomwa.
12. Marekebisho ya kifungu cha 32.
13. Marekebisho ya kifungu cha 36.
14. Marekebisho ya kifungu cha 49.
15. Marekebisho ya kifungu cha 101.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI, NAM. 15 YA 2013**

16. Kusomwa.
17. Marekebisho ya kifungu cha 2.
18. Marekebisho ya kifungu cha 14.
19. Marekebisho ya kifungu cha 90.
20. Marekebisho ya kifungu cha 116.
21. Kuongeza kifungu kipya cha 116A.
22. Kuongeza kifungu kipya cha 130A.
23. Kuongeza kifungu kipya cha 258A.

**SEHEMU YA SITA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KONDOMINIO YA ZANZIBAR, NAM. 10 YA 2010**

24. Kusomwa.
25. Marekebisho ya kifungu cha 2.
26. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 5.
27. Marekebisho ya kifungu cha 8.
28. Marekebisho ya kifungu cha 16.

29. Marekebisho ya kifungu cha 24.

30. Kufuta Sehemu ya Tano na kifungu cha 45.

**SEHEMU YA SABA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR, NAM. 12 YA 2018**

31. Kusomwa.

32. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 35.

**SEHEMU YA NANE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI, NAM.11 YA 2008**

33. Kusomwa.

34. Marekebisho ya kifungu cha 5.

**SEHEMU YA TISA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA BARABARA, NAM. 2 YA 2001**

35. Kusomwa.

36. Marekebisho ya kifungu cha 2.

37. Marekebisho ya kifungu cha 3.

38. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 6.

39. Kufuta Sehemu ya Tatu na kifungu cha 13.

**SEHEMU YA KUMI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO, NAM. 2 YA 2019**

40. Kusomwa.

41. Marekebisho ya kifungu cha 4.

42. Marekebisho ya kifungu cha 6.

43. Marekebisho ya kifungu cha 25.

44. Marekebisho ya kifungu cha 36.

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKONGWE, NAM. 4 YA 2010**

45. Kusomwa.

46. Marekebisho ya kifungu cha 4.

47. Marekebisho ya kifungu cha 6.

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005**

48. Kusomwa.

49. Marekebisho ya kifungu cha 29.

**SEHEMU YA KUMI NA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KAMISHENI YA ARDHI, NAM. 6 YA 2015**

50. Kusomwa.

51. Marekebisho ya kifungu cha 9.

52. Kuongeza kifungu kipya cha 9A.

**SEHEMU YA KUMI NA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTAMBUZI WA ARDHI, NAM. 8 YA 1990**

53. Kusomwa.

54. Kuongeza kifungu kipya cha 18A.

55. Marekebisho ya kifungu cha 22.

56. Marekebisho ya kifungu cha 25.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAJILI WA ARDHI, NAM. 10 YA 1990

57. Kusomwa.

58. Marekebisho ya kifungu cha 13.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA, NAM.2 YA 2011

59. Kusomwa.

60. Marekebisho ya kifungu cha 65.

**SHERIA NAM. 6 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

07, Novemba, **2023**

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2023 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**2**. Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zilivyoainishwa katika sehemu zake husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI WA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU NA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU, NAM. 10 YA 2009

Kusomwa.

**3**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**4**. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta tafsiri ya neno "ufadhili wa ugaidi" na kila linapojitokeza na kuweka badala yake tafsiri mpya ya neno "ufadhili wa kigaidi" kwa mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"ufadhili wa kigaidi" maana yake ni:

(a) utoaji wa fedha au rasilimali za kiuchumi au kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha au huduma zinazohusiana kwa:

(i) gaidi, kundi la kigaidi, taasisi ya kigaidi, tukio la kigaidi au kitendo cha kigaidi; au

(ii) mtu binafsi, kundi au taasisi inayohusika na ugaidi, kundi la kigaidi, taasisi ya kigaidi, tukio la kigaidi au kitendo cha kigaidi;

(b) kufanya muamala wa kifedha au kuwezesha muamala wa kifedha moja kwa moja au vyenginevyo, kwa lengo la kushughulikia mali inayomilikiwa au kudhibitiwa na gaidi, kundi la kigaidi au taasisi ya kigaidi;

(c) kufanya muamala wa kifedha au kuwezesha muamala wa kifedha moja kwa moja au vyenginevyo, kwa lengo la kushughulikia mali kwa niaba ya gaidi, kundi la kigaidi au taasisi ya kigaidi;

(d) kufadhili au kumuwezesha mtu yeyote binafsi au kundi la watu binafsi kusafiri kwenda nchi isiyokuwa nchi yake anayoishi au ya utaifa wake kwa lengo la kushiriki katika tukio la kigaidi, mafunzo ya kigaidi au kitendo cha kigaidi kwa lengo la kufanya, kutekeleza, kupanga au kuandaa vitendo vya kigaidi moja kwa moja au vyenginevyo;

(e) kuwapanga au kuwaelekeza watu wengine kufanya kitendo chochote katika aya ya (a), (b), (c) au (d) au kushiriki katika matendo hayo kama mshirika; au

(f) kujaribu kufanya vitendo vyovyote katika aya ya (a), (b), (c), (d) au (e)."

Marekebisho ya kifungu cha 10C.

5. Kifungu cha 10C cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Mtoa taarifa, wakati anapofanya uchunguzi wa utambuzi wa mteja:

(a) atachukua na atahakiki taarifa za mmiliki mnufaika wa mwisho wa mtu, taasisi au kwa utaratibu wa kisheria; na

(b) kwa upande wa mtu mwenye wadhifa maalumu, atafanya uchunguzi wa kawaida kama ilivyoelezwa chini ya Sheria hii na atatakiwa:

(i) kuwa na mifumo sahihi ya usimamizi wa viashiria hatarishi ili kubaini kama mteja ni mtu mwenye wadhifa maalum;

(ii) kupata idhini ya uongozi wa juu kwa ajili ya kuanzisha uhusiano wa kibiashara na mteja huyo;

(iii) kuchukua hatua zinazofaa ili kutambua chanzo cha mali na fedha; na

(iv) kufanya ufuatiliaji wa kina katika mahusiano hayo."

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Mtoa taarifa anaweza, kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Kanuni, kutegemea taarifa za utambuzi wa mteja zilizofanywa na mtoa taarifa mwengine."

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR, NAM. 3 YA 2015

Kusomwa.

**6.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, Nam. 3 ya 2015, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

7. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza ufafanuzi wa maneno mapya kwa mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"Matumizi salama ya viumbe hai" maana yake ni uepukaji wa hatari unaohusu ulinzi wa mazingira na afya ya binaadamu na wanyama ambayo inatokana na matokeo ya utafiti na biashara ya viumbe hai vilivyofanyiwa mabadiliko ya vinasaba;

"Biashara ya kaboni" maana yake ni kununua na kuuza au kuhamisha kaboni iliyoidhinishwa au kuthibitishwa katika utoaji, upunguzaji na uondoaji kwa mujibu wa Viwango vya Kaboni vya Kimataifa;

"Kiumbe kilichofanyiwa mabadiliko ya vinasaba" maana yake ni kiumbe chochote ambacho kimeongezewa sifa za vinasaba kutoka uasilia wake kwa kutumia mbinu za bioteknolojia ya kisasa;

"Uhariri wa vinasaba" maana yake ni mabadiliko ya vinasaba vya viumbe hai kwa kuingiza, kuweka mbadala au kufuta mpangilio wa vinasaba kwa lengo la kuimarisha baadhi ya sifa za mmea, mnyama au kutibu maradhi ya kimaumbile;

"Bioteknolojia ya kisasa" maana yake ni mbinu za bioteknolojia ya kisasa kwa ajili ya kubadilisha vinasaba na kuunganisha seli kwa kutumia mbinu zisizokuwa za kawaida.

Kuongeza kifungu kipya cha 64A.

**8**. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 64A mara baada ya kifungu cha **64** kama ifuatavyo:

"Usimamizi wa viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya vinasaba.

**64A**.-(1) Mtu ambaye anakusudia kushughulikia, kuingiza au kusafirisha viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya vinasaba au bidhaa zinazotokana na hayo au kufanya uhariri wa vinasaba atatakiwa kuomba kibali kwa Waziri kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Mtu ambaye anashughulikia, anaingiza au anasafirisha viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya vinasaba au bidhaa zinazotokana na mabadiliko hayo atakuwa na wajibu wa jumla wa kuhakikisha kwamba, viumbe hivyo haviathiri, havisababishi majeraha au haviathiri mazingira na afya ya binaadamu au wanyama ikijumuisha athari za uchumi kwa jamii, utamaduni na mila.

(3) Mtu ambaye anakiuka masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Hamsini za Kitanzania au kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka kumi au adhabu zote mbili faini na kifungo."

Kuongeza kifungu kipya cha 69A.

**9.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 69A mara baada ya kifungu cha 69 kama ifuatavyo:

Hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**69A**. Waziri, kwa kushauriana na Wizara husika:

(a) atachukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, hususani athari za mabadiliko ya tabianchi na hatua za kuhimili mabadiliko hayo;

(b) atatoa miongozo kila baada ya kipindi kwa Wizara na taasisi nyengine zozote kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake zinazotokana na ongezeko la joto duniani;

(c) atazitaka Wizara na idara zinazojitegemea kuweka mikakati na mipango ya utekelezaji kwa ajili ya kushughulikia mabadiliko ya tabianchi pamoja na skuli na taasisi za elimu ya juu kuingiza masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mitaala yao;

(d) atafanya mapitio na kupitisha hatua zozote za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinazochukuliwa na taasisi yoyote, kampuni, sekta au mtu binafsi, ikiwa kutoka ndani au nje ya nchi ikijumuisha taasisi zote zinazohusiana na matumizi ya ardhi, maji, misitu au mifumo yoyote ya ikolojia ndani ya Zanzibar katika kupunguza gesi joto; na

(e) ataratibu shughuli za biashara ya kaboni."

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 86.

**10**. Kifungu cha 86 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 86 kama ifuatavyo:

"Kanuni.

**86.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni kuhusiana na:

(a) usimamizi wa ukanda wa pwani;

(b) usimamizi endelevu wa maliasili zisizorejesheka;

(c) tathmini ya athari za kimazingira;

(d) mikakati ya tathmini ya kimazingira;

(e) bioanuwai;

(f) usalama wa viumbe hai;

(g) mabadiliko ya tabianchi;

(h) usimamizi wa biashara ya kaboni;

(i) ukingaji wa uchafuzi wa mazingira na usimamizi wa taka;

(j) usimamizi wa maliasili maji; na

(k) mambo mengine yoyote yanayohusiana na mazingira."

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA (UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI) MAFUTA NA GESI ASILIA, NAM. 6 YA 2016

Kusomwa.

**11**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya (Utafutaji na Uchimbaji) Mafuta na Gesi Asilia, Nam. 6 ya 2016, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 32.

**12**. Kifungu cha 32 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta maneno "utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia" yaliyopo baina ya maneno "katika" na "kwa niaba" yaliyopo katika kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake maneno "shughuli za mafuta"; na

(b) kuongeza maneno "na sheria nyengine yoyote" mwishoni mwa kifungu kidogo cha (2).

Marekebisho ya kifungu cha 36.

**13**. Kifungu cha 36 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kukibadilisha kifungu cha 36 kuwa 36(1);

(b) kufuta neno "kwa" baina ya maneno "kitatolewa" na "kipindi" yaliyopo katika kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake maneno "hadi kufikia"; na

(c) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka inaweza, kwa maslahi ya umma na kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii, kuongeza muda wa kibali cha awali pale itakapoona inafaa."

Marekebisho ya kifungu cha 49.

**14**. Kifungu cha 49 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, Waziri anaweza, baada ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi, kuingia katika majadiliano ya moja kwa moja na kampuni yoyote kwa ajili ya kumpatia eneo husika baada ya kuwasilisha maombi na kuonesha uwezo wa kifedha na utaalamu."

Marekebisho ya kifungu cha 101.

**15**. Kifungu cha 101 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta maneno "kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Pili" yaliyopo mwisho wa kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake maneno "kwa Serikali kwa mujibu wa mkataba wa mafuta na gesi asilia baada ya kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi"; na

(b) kufuta maneno "Jadweli la Pili" yaliyopo mwisho wa kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake maneno "kwa mujibu wa mkataba wa mafuta na gesi asilia baada ya kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi."

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI, NAM. 15 YA 2013

Kusomwa.

**16**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Makampuni, Nam. 15 ya 2013, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama."

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**17**. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza ufafanuzi wa maneno mapya kwa mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"mmiliki mnufaika" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009;

"mamlaka yenye uwezo" ina maana kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009;

"mtu mwenye wadhifa maalumu" ina maana kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009."

Marekebisho ya kifungu cha 14.

**18**. Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kukibadilisha kifungu cha 14 kuwa 14(1);

(b) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kanuni za Ushirikiano za Kampuni zitawasilishwa na taarifa kwa namna ilivyoelezwa na itajumuisha:

(a) jina kamili na anuani au ofisi iliyosajiliwa ya mtu au watu ambao ni:

(i) mkurugenzi wa mwanzo au wakurugenzi wa kampuni; na

(ii) katibu wa mwanzo au makatibu wa pamoja wa kampuni na ikiwa mkurugenzi au wakurugenzi wa mwanzo, taarifa za wakurugenzi wengine wowote wa miaka mitano kutoka tarehe ambayo taarifa imewasilishwa kwa Mrajis;

(b) kumbukumbu sahihi na za kisasa za wamiliki wanufaika wa Kampuni hiyo ambayo itajumuisha:

(i) jina kamili, ikijumuisha jina lolote la zamani au majina mengine;

(ii) tarehe na mahali alipozaliwa;

(iii) nambari ya simu;

(iv) utaifa, nambari ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, nambari ya Kitambulisho cha Taifa au nambari ya hati ya kusafiria;

(v) anuani ya makaazi, posta na barua pepe (ikiwa ipo);

(vi) sehemu anayofanya kazi na nafasi inayoshikiliwa;

(vii) asili ya riba ikijumuisha maelezo ya kisheria, kifedha, usalama, mgao wa faida au mpangilio usio rasmi unaosababisha umiliki wa mnufaika; na

(viii) kiapo au uthibitisho iwapo mmiliki mnufaika ni mtu mwenye wadhifa maalumu au la."

Marekebisho ya kifungu cha 90.

**19**. Kifungu cha 90 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya (4) na (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Hati ya hisa haitatolewa au kuhaulishwa kwa utoaji wa hati isipokuwa kwa idhini ya Mrajis.

(5) Mrajis atatunza kumbukumbu za hati za hisa zilizotolewa au kuhaulishwa chini ya Sheria hii."

Marekebisho ya kifungu cha 116.

**20**. Kifungu cha 116 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Kampuni, katika daftari lililotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1), itaingiza taarifa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 14 cha Sheria hii."

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (2), (3) na (4) kuwa vifungu vidogo vya (3), (4) na (5) kwa mpangilio wake; na

(c) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (6) mara baada ya kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"(6) Endapo kutakuwa na mabadiliko katika umiliki wa mnufaika wa kampuni, kampuni itatoa taarifa kwa Mrajis ndani ya siku thelathini ya mabadiliko hayo."

Kuongeza kifungu kipya cha 116A.

**21**. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 116A mara baada ya kifungu cha 116 kama ifuatavyo:

"Daftari la kumbukumbu la wamiliki wanufaika.

**116A.-**(1) Mrajis ataanzisha na kutunza daftari la kumbukumbu la wamiliki wanufaika ambalo litakuwa na:

(a) taarifa iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 116(2) cha Sheria hii; na

(b) taarifa zinazohusiana na taasisi ya kisheria ambayo itajumuisha:

(i) jina la taasisi;

(ii) anuani ya Ofisi kuu;

(iii) utambulisho wa wakurugenzi, wanahisa na wamiliki wanufaika;

(iv) uthibitisho wa kuingizwa au ushahidi wa hadhi ya kisheria na fomu ya kisheria; na

(v) taarifa nyengine muhimu ili kuamua umiliki na udhibiti wa taasisi ya kisheria.

(2) Taarifa juu ya wamiliki wanufaika wa kampuni iliyopo kwa Mrajis katika daftari la wamiliki wanufaika itapatikana na mamlaka yenye uwezo."

Kuongeza kifungu kipya cha 130A.

**22.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 130A mara baada ya kifungu cha 130 kama ifuatavyo:

"Kumbukumbu za mmiliki mnufaika.

**130A.**-(1) Kampuni ambayo ina mmiliki mnufaika, itaingiza taarifa za mmiliki mnufaika katika daftari la kumbukumbu lake kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 14(2)(b) cha Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kampuni itawasilisha kwa Mrajis kumbukumbu za mwaka za wamiliki wanufaika wake."

Kuongeza kifungu kipya cha 258A.

**23.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 258A mara baada ya kifungu cha 258 kama ifuatavyo:

"Uwasilishaji wa taarifa za umiliki wa mnufaika.

**258A.**-(1) Kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria hii kabla ya tarehe 1 Oktoba, 2023, ndani ya miezi sita kutoka tarehe 1 Oktoba, 2023, italazimika kufuata masharti ya kifungu cha 14(2)(b) cha Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti Rasmi, kuongeza muda wa kufuata masharti ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki."

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KONDOMINIO YA ZANZIBAR, NAM. 10 YA 2010

Kusomwa.

**24**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kondominio ya Zanzibar, Nam. 10 ya 2010, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**25**. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta tafsiri ya maneno "Bodi".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 5.

**26**. Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 5 kama ifuatavyo:

"Uteuzi wa Mrajis.

**5.**-(1) Kutakuwa na Mrajis wa Kondominio atakayeteuliwa na Waziri.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mrajis wa Kondominio ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza ya sheria kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu usiopungua miaka mitatu katika masuala ya kondominio; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu."

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**27**. Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "Bodi" katika kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake neno "Waziri".

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**28**. Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta maneno "Bodi au" katika kifungu kidogo cha (1)(b) na kuweka badala yake neno "Mrajis"; na

(b) kufuta neno "Bodi" katika kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake neno "Mrajis".

Marekebisho ya kifungu cha 24.

**29**. Kifungu cha 24 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "Bodi" katika kifungu kidogo cha (2) na (3) na kuweka badala yake neno "Mrajis".

Kufuta Sehemu ya Tano na kifungu cha 45.

**30**. Sehemu ya Tano na kifungu cha 45 vya Sheria Mama vinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(a) Sehemu ya Tano na kifungu cha 45 vya Sheria Mama vinafutwa;

(b) Kuzipa nambari mpya Sehemu ya Sita kuwa Sehemu ya Tano na kifungu cha 46 kuwa cha 45 na kufuata mpangilio wake.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR, NAM. 12 YA 2018

Kusomwa.

**31**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Nam. 12 ya 2018, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 35.

**32.** Kifungu cha 35 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 35 kama ifuatavyo:

"Wajibu wa taasisi za Serikali.

35.-(1) Taasisi zote za Serikali zitawajibika kupata huduma za uchapaji, vifaa vya kuandikia na vifaa vya ofisi kutoka kwa Wakala.

(2) Endapo Wakala utakuwa hauna uwezo wa kutoa huduma zilizoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mtendaji anaweza, kwa maandishi, kuruhusu taasisi ya Serikali husika kuchapisha au kununua vifaa vya kuandikia au vifaa vya ofisi nje ya Wakala.

(3) Bila ya kujali masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, taasisi za Serikali zinaweza kupata huduma ya vifaa vya kuandikia na vifaa vya ofisi kutoka taasisi nyengine yoyote iliyopewa uwezo na sheria.

(4) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki na masharti ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016, taasisi zote za Serikali zitatumia njia ya ununuzi kwa mzabuni mmoja."

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI, NAM.11 YA 2008

Kusomwa.

**33**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**34**. Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa:

(a) kuongeza aya mpya ya (c) mara baada ya aya ya (b) kama ifuatavyo:

"(c) kutoa huduma za vifaa vya kuandikia na vifaa vya ofisi"; na

(b) kuipa nambari upya aya ya (c) kuwa aya ya (d).

## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA BARABARA, NAM. 2 YA 2001

Kusomwa.

**35**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Barabara Zanzibar, Nam. 2 ya 2001, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**36**. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta tafsiri ya maneno "Bodi" na "mpokeaji wa mapato"; na

(b) kuongeza tafsiri ya neno "Katibu Mkuu" katika mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu wa Wizara inayohusiana na Fedha".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**37**. Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta neno "Bodi" katika kifungu cha 3 na popote linapojitokeza na kuweka badala yake neno "Katibu Mkuu".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 6.

**38**. Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 6 kama ifuatavyo:

"Kuhamishwa kwa fedha za Mfuko.

**6.** Katibu Mkuu atahamisha fedha zote zilizokusanywa na Mfuko kwenda katika hesabu ya Wakala wa Barabara Zanzibar kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa mujibu wa mpango kazi wa Wakala wa Barabara Zanzibar."

Kufuta Sehemu ya Tatu na kifungu cha 13.

**39**. Sehemu ya Tatu na kifungu cha 13 vya Sheria Mama vinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(a) Sehemu ya Tatu na kifungu cha 13 vya Sheria Mama vinafutwa;

(b) Kuzipa nambari mpya Sehemu ya Nne kuwa Sehemu ya Tatu na kifungu cha 14 kuwa cha 13 na kufuata mpangilio wake.

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO, NAM. 2 YA 2019

Kusomwa.

**40**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, Nam. 2 ya 2019, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**41**. Kifungu cha 4(2) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta aya ya (a).

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**42**. Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya ya (c) na (f); na

(b) kufuta maneno "mafunzo ya kiufundi" katika aya (e) yaliyopo baina ya maneno "kutoa" na "kwa" na kuweka badala yake maneno "mafunzo ya kitaalamu."

Marekebisho ya kifungu cha 25.

**43**. Kifungu cha 25 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta vifungu vidogo vya (2) na (3) na kuweka badala yake vifungu vidogo vipya vya (2) na (3) kama ifuatavyo:

"(2) Mkuu wa idara na mkuu wa kitengo atateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao na watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

(3) Mkuu wa divisheni atateuliwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa kuzingatia sifa na uzoefu wake na atawajibika kwa mkuu wa idara husika."

Marekebisho ya kifungu cha 36.

**44**. Kifungu cha 36 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "ushauri wa kiufundi" yaliyopo baina ya maneno "kuomba" na "kwa Wakala" katika kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake maneno "ushauri wa kitaalamu."

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKONGWE, NAM. 4 YA 2010

Kusomwa.

**45**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Uhifadhi na Maendeleo ya Mji Mkongwe, Nam. 4 ya 2010, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4

**46**. Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno "maeneo ya maegesho" baina ya maneno "maeneo ya wazi," na "bustani" katika aya ya (d).

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**47**. Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza maneno "ikijumuisha usimamizi wa taka" baina ya maneno "mazingira" na "ndani ya" katika aya ya (e); na

(b) kuingiza maneno "na leseni" baina ya maneno " kibali" na "ndani ya" katika aya ya (f).

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

Kusomwa.

**48**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**49**. Kifungu cha 29(4) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta aya ya (b) na kuweka badala yake aya mpya ya (b) kama ifuatavyo:

"(b) ajira yake imefikia ukomo au amepoteza ajira kwa sababu yoyote ile isipokuwa kuacha kazi kwa hiari au kuachishwa kazi kwa makosa ya rushwa, ubadhirifu, wizi, makosa ya kinidhamu au kwa kushiriki katika siasa kwa mujibu wa sheria husika."

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KAMISHENI YA ARDHI, NAM. 6 YA 2015

Kusomwa.

**50**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kamisheni ya Ardhi, Nam. 6 ya 2015, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**51**. Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya mpya ya (b) mara baada ya aya ya (a) katika kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(b) Katibu Mtendaji;"

(b) kufuta neno "tatu" baina ya neno "mwengine" na "mjumbe" katika aya ya (e) na kuweka badala yake neno "mbili";

(c) kufuta aya ya (f); na

(d) kupanga upya aya **za** (b), (c), (d) na (e) kuwa aya za (c), (d), (e) na (f) kwa mpangilio wake.

Kuongeza kifungu kipya cha 9A.

**52**. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 9A mara baada ya kifungu cha 9 kama ifuatavyo:

"Katibu wa Bodi.

**9A**.-(1) Bodi itamteua mtu ambaye ni mfanyakazi wa Kamisheni kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au ana sifa ya kuwa Katibu wa Shirika; na

(b) ana uzoefu wa kazi usiyopungua angalau miaka mitatu katika utumishi wa umma.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na:

(a) kwa kushauriana na Mwenyekiti, ataandaa ajenda za kikao cha Bodi;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza kumbukumbu sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(e) atatekeleza kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria hii."

**SEHEMU YA KUMI NA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTAMBUZI WA ARDHI, NAM. 8 YA 1990**

Kusomwa.

**53**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utambuzi wa Ardhi, Nam. 8 ya 1990, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 18A.

**54**. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 18A mara baada ya kifungu cha 18 kama ifuatavyo:

"Usajili wa utambuzi.

**18A**.-(1) Mtu yeyote ambaye anawasilisha hati ya matumizi ya ardhi iliyohakikiwa au mkataba wa ukodishaji wa ardhi atatambuliwa na Ofisa kumbukumbu kama ndiye mmiliki wa eneo la ardhi husika lililotambuliwa na hatolazimika kufuata taratibu zilizowekwa chini ya vifungu vya 21, 22, 23, 24 na 25 vya Sheria hii.

(2) Ofisa Mtambuzi atahakiki na kuthibitisha kumbukumbu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na atawasilisha barua ya utambuzi kwa Mrajis kwa ajili ya usajili kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Ardhi, Nam.10 ya 1990."

Marekebisho ya kifungu cha 22.

**55**. Kifungu cha 22 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "tisini" liliopo baina ya maneno "ndani" na "siku" na kuweka badala yake neno "thelathini".

Marekebisho ya kifungu cha 25.

**56**. Kifungu cha 25 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "tisini" liliopo baina ya maneno "baada ya kumaliza" na "siku" na kuweka badala yake neno "thelathini".

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAJILI WA ARDHI, NAM. 10 YA 1990

Kusomwa.

**57**. Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usajili wa Ardhi, Nam. 10 ya 1990, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 13.

**58**. Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno "18A na" baina ya maneno "kifungu" na "25".

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA, NAM.2 YA 2011

Kusomwa.

**59.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 65.

**60**. Kifungu cha 65 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Uhamisho wowote utakaozidi mwaka mmoja utachukuliwa kama uhamisho ambao mafao yote na maslahi anayostahiki kupewa atapewa isipokuwa uhamisho chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki.";

(b) kuongeza maneno "na uhamisho huo utachukuliwa kama ni likizo bila ya malipo isipokuwa kwa wale ambao wapo chini ya mfumo wa malipo ya mishahara ya Serikali" mwisho wa kifungu kidogo cha (5).

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 4 Oktoba, 2023.

..........................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

*Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.*